USAFIRI KWENYE GARIMOSHI LA MAUTI

© Moses C. Onwubiko

"Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake" (Yohana 15:13).

UTANGULIZI

Hebu jione kuwa wewe ni abiria kwa garimoshi linaloelekea kambi ya mauti. Abiria wote ndani ya hilo garimoshi, wewe ukiwa mmoja wao, mumehukumiwa na munaelekezwa kwenye hiyo kambi ya mauti ili muuawe.

Ikiwa umesalia mwendo mfupi ili kufika tamati, kijana wa kiume akaonekana akiwa amesimama njiani, akipeperusha bendera nyekundu, akiashiria gari lisimame. Mwangalizi wa abiria, kwa shida, akafaulu kusimamisha garimoshi kwa ghafla na kishindo kikubwa.

Wasimamizi wa garimoshi walitoka nje kwa haraka wakamuendea na kumhoji yule kijana wa kiume ili wapate kuelewa ombi lake la ajabu, eti alitaka kufa kwa niaba ya kila mmoja aliye hukumiwa! "Niko hapa kusitisha maagizo ya kuuawa," huyo kijana wa kiume akatangaza kwa ujasiri.

Kwa haraka mno, wasimamizi hawa walioshangazwa, wakapeleka habari ya tukio hili lisilo la kawaida kwa hakimu aliyetoa sharti ya maagizo ya hukumu.

Baada ya yule kijana wa kiume kuchunguzwa na kuhojiwa kwa muda, hakimu alimruhusu afe badala ya abiria wote waliokuwa wameandikiwa hatima ya madhara, kwa sababu kumbukumbu ya habari ya maisha yake haikuwa na dalili ya uhalifu wowote. Kulingana na taarifa yake yote hakuwa na hatia yoyote, lakini alikuwa amejitolea kwa hiari kuchukua hukumu yao juu ya maisha yake.

Upendo Wake Kwa Wenye Hatia Unaonyeshwa Dhahiri

Watu wote waliokuwa ndani ya garimoshi, wewe ukiwa mmoja wao, mnatazama akielekezwa kuuawa. Aliteswa na kudhulumiwa kwa niaba ya wote walio nusurika kifo.

Ningependa uchukue muda mfupi na ufikirie sana kuhusu ishara aina hii; kuwa haieleweki kwa urahisi kwamba mtu anaweza kujitolea kamili kwa niaba ya walio hukumiwa.

Wakati kijana huyu wa kiume asiye na hatia anapoangikwa juu ya mti katika kambi ya kifo, anapiga mayowe kwa uchungu na kuita msaada kwa sauti kubwa ila hapati usaidizi. Kisha akavuta pumzi mara ya mwisho naye akakata roho. Kwa nini? Ili walio ndani ya garimoshi

waachiliwe huru waishi. Basi hakimu anatoa uamuzi kuhusu yale mambo yanayo wapasa wale watu walio kwa lile garimoshi kutenda, ili waachiliwe huru kutokana na kifo cha yule kijana wa kiume aliyejitoa kuwa dhabihu.

Ukweli Halisi

Hii sio hadithi tu bali ni mfano. Biblia inanakili wazi ya kwamba:

> Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu [kiwango] wa Mungu (Warumi 3:23).

> Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti... (Warumi 6:23a).

Uamuzi huu wa mahakama kuu ya mbinguni waonyesha kwamba kila mtu ana hatia ya dhambi, na kuwa wote lazima wahukumiwe kwenda jehanamu, wakiwa wametenganishwa na Mungu milele. Kila mtu, bila kubaguliwa, yupo chini ya hukumu ya Mungu - anasafiri kwenye garimoshi la mauti akielekea kuangamizwa milele.

Jitihada Za Mwanadamu

Biblia imetoa mwelekeo kukanusha jaribio la mwanadamu kujihesabia haki mbele za Mungu. Huenda mmoja akasema, “Hakika, mimi najaribu kuwa mtu mwema.” Biblia inasema,

> ... hakuna mtenda mema, la! hata mmoja (Warumi 3:12b).

Hiyo inamuacha wapi mtu huyu? Ijapokuwa mtu mwingine anaweza kushindana akisema, “Nimekuwa nikijaribu kuzitunza na kuzitenda amri za Mungu,” kwa hilo pia Biblia inajibu:

> Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote (Yakobo 2:10).

Swali linalotatiza ni hili, ni amri ngapi za Mungu anazohitajika mwanadamu kuzitunza ili aweze kukubalika mbinguni? Jibu ni amri zote! Mtu akikosea hata kidogo kwa amri moja ina maana kuwa amekosea katika amri zote. (***Yakobo 2:10)***. Ni nani basi anayeweza kuwa mkamilifu kwa zote? Nani anayeweza kukaa siku nzima, au juma lote au mwaka mzima bila kufanya kosa lolote katika amri za Mungu? Ukweli ni kwamba:

> ... hakuna mwenye haki hata mmoja (Warumi 3:10b).

Mtu anaweza kuendelea kushindana zaidi akisema ya kwamba, yeye anajaribu kuishi maisha ya haki. Hapo tena Biblia inasema:

> Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi; sisi sote twanyauka kama jani, na maovu yetu yatuondoa, kama upepo uondoavyo (Isaya 64:6).

Bila shaka, hii si habari njema kwa mtu yeyote. Kila jitihada za mwanadamu za kupokea idhini ya Mungu zimefutiliwa mbali. Basi tunabaki na nini?

Hamna Kitu!

Je, Mungu anapokanusha hivi ina maana kwamba hakuna mwanadamu yeyote yule anayeweza kuenda mbinguni? La hasha! Ina maana kwamba kila juhudi ya kila mwanadamu haina manufaa. Tumaini la pekee na suluhisho la pekee ni Neema ya Mungu.

Mwanadamu Katika Hali Yake Ya Kutojiweza

Bwana Mungu akiwa yeye ndiye Muumbaji, ni Mtakatifu. Yeye ni mwenye haki kamilifu na Mungu mwenye hukumu halisi. Katika hali yake ya utakatifu, hawezi kamwe kushirikiana na dhambi wala wenye dhambi. ***"Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake." (1 Yohana 1:5)***. Kama alivyo Mungu mwenye haki halisi, hawezi na hataweza kuruhusu dhambi kufanyika bila kutoa adhabu. Hakuna kwa vyovyote vile mwanadamu yeyote asiye mkamilifu, anaweza kuwa na uhusiano na Mungu mkamilifu; haiwezekani kamwe kulingana na juhudi za mwanadamu.

> ***...kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana. (Mathayo 19:26b).***

Kwa hivyo, mwanadamu katika harakati zake za kujitahidi, kwa nguvu zake zote, hawezi wala hataweza kamwe kufikia kiwango cha Mungu katika utakatifu wake. Mtu anajidhania kwamba yeye ni mwema, ila Mungu naye anasema ***"... hakuna mtenda mema, la! hata mmoja." (Warumi 3:12b)***. Mtu mwingine anafikiri eti yeye anaishi maisha mazuri. Mungu anajibu akisema, ***"... hakuna mwenye haki hata mmoja." (Warumi 3:10b)***. Mwingine pia anafikiri eti anaweza kuhesabiwa haki kwa kutunza sheria za Mungu. Huyo pia Mungu anamjibu akisema,

> ***... maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki." (Wagalatia 2:16b).***

Kwa hakika, mwanadamu amepungukiwa na mbinu za kujaribu kujiepusha na hukumu ya Mungu, iliyo ya kiungu, ambayo imehesabiwa kwa wote. ***"kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utuku wa Mungu," (Warumi 3:23).*** Hakuna njia ya kuepuka hukumu yake. Wote tayari wamehukumiwa, wameshutumiwa na kustahili kifungo cha kutupwa katika jehanamu ya milele. Haijalishi vile mtu anavyoweza kujitahidi kwa nguvu zake mwenyewe, haiwezekani kamwe kuepuka hatima hii. Je! hii ina maana ya kwamba hakuna

matumaini ya kuepuka hukumu ya Mungu? La! sivyo kabisa. Mungu ana mpango mmoja tu wa kuwezesha mtu kuepuka, na huu ni mpango wa Neema. Uufuate mpango huu nawe utakuwa huru ama uukatae nawe ukabiliane na ghadhabu ya Mungu milele. ***"Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia." (Yohana 3:36.)***

Habari Njema

Mwanadamu alipokuwa akijaribu kuepuka hukumu ya Mungu kwa juhudi zake mwenyewe, mtu mmoja alikuja kumuokoa. Mtu huyu ni Yesu Kristo, mwana wakipekee wa Mungu. Alijitolea kama mwana asiyekuwa na lawama yoyote, anayestahili kuchukua hukumu ya kifo cha mwanadamu juu yake mwenyewe. Kwa habari kuhusu mtu huyu wa kipekee, Yesu Kristo, mtume Yohana anasema hivi:

> ***...Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. (Yohana 1:29b)***.

Alichukua adhabu ya dhambi zetu. Mtume Petro anaongezea akisema;

> Yeye [Yesu Kristo] mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa (1 Petro 2:24).

Mtume Paulo naye anatangaza akisema,

> Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa [badala ya mwanadamu] kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. (Warumi 5:8).

Deni la dhambi limelipwa kwa ukamilifu, mara moja tu kwa watu wote, ***"wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele." (Waebrania 9:12).***

Habari Hii Njema Yaweza Kuwa Nzuri Kiasi Gani?

Gharama yote ya deni la mauti limekwisha kulipwa kwa ukamilifu. Kizuizi katikati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu asiyekuwa mwenye haki kimeondolewa. Dhambi ilimtenganisha mwanadamu na Mungu "***lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia" (Isaya 59:2).*** Yesu Kristo aliondoa kizuizi hiki alipokufa msalabani badala ya wanadamu. Laana iliyokuwa imewekwa juu ya mwanadamu kwa kutokuwa na uwezo wakuitunza Sheria ya Mungu, ilishughulikiwa pia na hicho kifo kibadala:

> Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti ***(Wagalatia 3:13).***

Yesu Kristo pekee yake, bila kuhusishwa kwa mwanadamu yeyote, alifanya amani na Mungu; "***Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu," (1 Timotheo 2:5)***. Tatizo la ukuta mkubwa usiopitika, shida ya kushindwa kwa mwanadamu kufuata Sheria za Mungu na jitihada za mwanadamu sizizo tosheleza matakwa ya Mungu zilitatuliwa zote pale msalabani na Yesu Kristo.

> Akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu, akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani (Wakolosai 2:14).
>
> Kwa maana yeye [Yesu Kristo] ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani (Waefeso 2:14-15).
>
> Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa [badala] kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi [maadui wa Mungu] (Romans 5:8).

Kuondoka Kusio Weza Kusahaulika

Rudi ufikirie ule mfano wa garimoshi linaloelekea kwa kambi ya mauti. Baada ya yule mtu asiyekuwa na hatia kutoa maisha yake, hakimu alitoa sharti ya kwamba waliotaka kuondoka kwenye garimoshi iliwabidi wapitie ule mlango walioelekezwa. Kuondoka huku kunatukuza kifo cha mtu huyu, asiyekuwa na hatia, ambaye alikufa badala ya wale abiria. Ni kuondoka kwa ajabu kulioje! Fikiria kuhusu kile kinachoweza kuwa kinaendelea katika mawazo ya hawa waliohukumiwa, wakati wanapotii amri ya hakimu na kuondoka wapate kuwa huru. Katika mfano, Mungu ametoa amri kutoka mahakama yake mbinguni. Taratibu ya pekee inayokubalika kwa haki kamilifu ya Mungu ni kuingia ukitumia mlango mmoja tu. Hakuna maafikiano kuhusu njia hii bali maagizo ya Mungu ni sahihi. Iliwabidi abiria wa garimoshi, waondoke kupitia mlango mmoja tu. Yeyote yule anayetamani kuingia mbinguni ni sharti atumie ule mlango teule wa Mungu.

Njia Ya Kuingia Mbinguni

Kuhusu uamuzi wa Mungu, Yesu Kristo mwenyewe anasema!

> "... Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, [mbinguni] ila kwa njia ya Mimi." (Yohana 14:6b).

Luka mtakatifu anaongezea akisema,

> Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo. (Matendo ya Mitume 4:12).

Hii inatilia mkazo kwamba, isipokuwa kupitia kwa Yesu Kristo, hakuna mwanadamu yeyote anayeweza kuokolewa wala kamwe kwenda mbinguni. Yesu Kristo mwenyewe anadhibitisha haya

> ***"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6)***

na hakuna njia ya mkato inayotosha. Mungu anamaanisha kile anachosema. Tafuta ule mlango na uingie, au ufungiwe kuingia mbinguni milele.

Jinsi Ya Kuokolewa

Kuna njia moja tu ya kwenda mbinguni nayo ni kupitia Yesu Kristo ambaye anasema:

> ***"Mimi ndimi mlango; mtu akiingia kwa mimi, ataokoka..." (Yohana 10:9a)***.

Je! ni vipi mtu ataingia mlango ule asiouona? Kwa kuwa Yesu Kristo ndiye mlango; njia ya pekee ya kuingia ni kwa imani tu katika Yesu Kristo pekee. Mlango mmoja, njia moja, imani moja ndani ya Kristo pekee. Imani kiwango gani? Ndogo sana kama "... punje ya haradali ..." (Mathayo 17:20).

Kielelezo cha Imani: Katika agano la kale wana wa Israeli walimuasi Mungu. Mungu katika hukumu ya haki yake alizituma nyoka za moto miongoni mwa watu. ***"BWANA akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa." (Hesabu 21:6).*** Zile nyoka ziliwauma na kuwaua watu wa aina yeyote. Wana wa Israeli, katika mateso yao, waliungama dhambi zao kwa Mungu. Mungu angeziruhusu nyoka zile ziwaangamize wana wa Israeli walioasi, lakini hakufanya hivyo. Je, Mungu alifanya nini badala yake? Katika Neema yake isiyo na kifani, alimuambia Musa

> '... jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi' (Hesabu 21:8)**.**

Basi Musa alifanya kulingana na vile alivyo amuriwa na Mungu. Unaona! Musa alifuata amri ya Mungu sawa sawa kabisa. Ndipo ikawa ni zamu ya wana wa Israeli kufuata maagizo ya Mungu kwa uangalifu, vile vile, kupitia Musa. Walikuwa na chaguo: kufanya tu vile Mungu alivyosema au wafe.

Kwa hakika, wale wote walioumwa, ambao hawakuikosoa Neema ya Mungu, wala hekima yake, au kunung'unika kuhusu urahisi wa maagizo ya Mungu bali kwa uwepesi walitazama yule nyoka

aliyetengenezwa na Musa, waliishi. (***Hesabu 21:8)***. Je! ni ya ajabu namna gani, ya kutisha namna gani, ni rahisi namna gani ilivyokuwa Neema ya Mungu kwa wana wa Israeli wote; ilikuwa rahisi sana hadi watu wote wazee kwa vijana wangemtazama tu yule nyoka na kuishi. Haikuwepo aina yoyote ya kazi ya ziada kwa maagizo yake ya Neema. Mungu hakuitaji ahadi kutoka kwa mwanadamu, mwanadamu kujipa sharti, kuwekwa wakfu au kurudia kuwekwa wakfu na mkusanyiko wa waumini, wala ubatizo au kulipa zaka. Je, ni suluhisho la Neema iliyo ya ajabu namna gani, kutoka kwenye mahakama ya Mungu wa upendo? Ni yule yule Mungu aliempa Musa maagizo miaka elfu kadha zilizopita, ametoa tena suluhisho nyingine rahisi kwa mwanadamu katika hali yake ya kutojiweza.

Mwana Wa Mungu Ameinuliwa Juu

> "Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa, ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye." (Yohana 3:14-15).

Yesu Kristo aliinuliwa juu msalabani aliposulubiwa. Kama vile tu wana wa Israeli walivyotazama yule nyoka aliyeinuliwa juu na Musa, wewe pia unaweza kutazama msalabani na kupitia imani tu katika Yesu Kristo uweze kupata uhakikisho, kutoka kwa Mungu mwenyewe, kuwa una uzima wa milele.

Kule jangwani, iliwabidi watazame nyoka tu. Lakini je! kutazama tu kuna ustahili gani? Hamna kabisa! Pale msalabani ni kuamini tu. Lakini tena, kuamini huku kuna ustahili gani? Hamna. Yesu Kristo pekee ndiye anaye stahili. Je! ilikuwa rahisi jinsi gani kwake Mungu kuutoa ukombozi kule jangwani, na je ni rahisi jinsi gani kwake Mungu kuutoa ukombozi wake sasa? Mungu hufanya mambo kuwa rahisi bali shetani pamoja na wanaoshirikiana na yeye hutatanisha toleo la Neema ya wokovu kutoka kwa Mungu. Wokovu ni jambo rahisi mno, ni rahisi tu kama "kuamini Yesu Kristo," wala sio "kuamini na kubatizwa", "kuamini na kujiunga na kanisa fulani", "kuamini na kuendelea kuamini zaidi", "kuamini na kutubu na kuamini tena" au "kuamini na kumfanya Yesu Kristo kuwa Bwana"; maana yeye tayari ni Bwana. Hakuna hali ya kujitolea inayofaa kuongezwa juu ya imani. Agizo la Mungu kuhusu wokovu limeelezwa dhahiri.

> Amwaminiye [hata wewe] Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini [amri ya kuamini] Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia (Yohana 3:36).
>
> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele (Yohana 3:16).
>
> Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini muwe na uzima kwa jina lake (Yohana 20:31)**.**

Uaminifu Wa Mungu

Je, inawezekana Mungu adanganye? La, hasha!

> Mungu si mtu, aseme uongo ... (Hesabu 23:19a).

Mungu akisema: “Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele ...” (na ndivyo alivyosema katika Yohana 3:36), hivyo ndivyo alivyomaanisha. Tena akisema: “...kila mtu amwaminiye (Yesu Kristo) asipotee...” (na ndivyo alivyosema katika Yohana 3:16), alimaanisha ya kwamba yeyote atakaye mtumainia Kristo hataenda Jehanamu. Ni rahisi hivyo tu. Kwa namna nyingine, Mungu akisema: “Mtu yeyote amwaminiye Yesu Kristo, na amfanye kuwa bwana, na abatizwe, na ajitolee kwake, hatapotea kamwe,” ni bora kufanya hayo yote iwapo kweli unalo tumaini la uzima wa milele. Faraja iliyoje, maana hasemi hivyo! Jambo moja ni dhahiri katika neno lake:

> ... mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka ... (Matendo ya Mitume 16:31).

Hii ni Neema ya Mungu ikitenda kazi.

Uamuzi Wako Mkubwa

Wakati huu, unaweza kufanya uamuzi mkubwa ambao utabadilisha mwelekeo wa maisha yako milele. Jinsi gani? Kwa urahisi tu ukimwambia Mungu Baba, kwa sauti au kimoyo-moyo, kwamba sasa unaamini katika Mwana wake alieinuliwa juu msalabani ili afe kwa niaba yako. Wakati unapoweka tumaini lako lote katika Kristo, basi umelitii neno la Mungu. Papo hapo, muujiza wa wokovu wako unaanza. Wakati wa ajabu jinsi gani katika maisha ya mwanadamu! Ni maisha iliyokombolewa kimiujiza na Neema ya Mungu milele.

> Kwa maana mmeokolewa kwa Neema, kwa njia ya imani... (Waefeso 2:8a).

Ni muujiza gani huu? Mungu kwa kubadilisha imani yako dhaifu na haki iliyooza, anakupa haki yake kamilifu, ***“ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti,” (Warumi 3:22)***, ambayo ni msingi wa kuhesabiwa haki. Baadhi ya mambo mengine, anakupa uzima wake wa milele. ***“Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia.” (Yohana 3:36)***. Papo hapo unamiliki haki ya Mungu. Pia unapata uzima wake ndani yako. Hivi vipawa vya Neema kutoka kwa Mungu, kwa mara ya kwanza katika maisha yako, vina kuhalalisha kuishi na Mungu mbinguni milele. Ulifanya nini kupokea moja wapo ya vitu hivi? Hakuna! Kwa hiyo, unaweza kufikia uamuzi bila pingamizi kwamba haukufanyia kazi wala kustahili wokovu pasipo Neema ya Mungu. Jumla ya mambo yote ni hivi: hauwezi boresha kile Mungu amefanya. Kazi ya Mungu ni kamilifu na haina majuto. ***“Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto, wala mwito wake.” (Warumi 11:29).***

Hii ndiyo Habari Njema. Fursa imepatikana. Uamuzi ni wako. Wokovu ni kwa imani ndani ya Kristo, na ni kwa Yesu Kritso pekee yake. Hili ndilo suluhisho la pekee kutoka kwa Mungu ili uweze kuepuka mauti ya milele. Kubali toleo lake la Neema na ubadilishwe, au ukatae toleo lake la pekee la Neema nawe utakabiliana na matokeo ya hukumu ya adhabu milele.

Uamuzi wa Mungu unadumu:

> Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia. (Yohana 3:36).

Chaguo ni lako mwenyewe; kwa hivyo:

Baba wa mbinguni, tunakushukuru kwa kipawa chako cha Neema; Mwanao aliyetolewa msalabani. Tunakushukuru kwa kufanya wokovu kuwa rahisi na upatikane kwa kila mtu. Tunawaombea wale ambao wamesoma ujumbe huu wa injili na hawajafanya uamuzi mkubwa kwa ajili ya maisha yao. Tunaomba ya kwamba wafikie kiwango cha kuelewa kikamilifu maana haswa ya kukubali au kukataa toleo Lako la wokovu wa milele. Tunakusihi Baba, uwape changamoto wale ambao hawajaamini katika Kristo kibinafsi ili waendelee kutafakari ujumbe huu. Katika jina la Yesu Kristo, Amina.

Kwa Wale Ambao Wameamini

Mungu anadai wale walioamini wapate kukua katika Neema ***"Lakini, kueni katika Neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele." (2 Petro 3:18)***. Anataka sana waendelee kuwa na njaa ya mafundisho ya kweli. ***"Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu." (1 Peter 2:2).***

MAOMBI (Kwa waaminio pekee)

> Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani (Wakolosai 4:2).
>
> ... Kuomba kwake mwenye haki [haki kupitia imani kwa Yesu Kristo] kwafaa sana, akiomba kwa bidii. (Yakobo 5:16b).
>
> Mkituombea na sisi pia, [akiwemo Musa pamoja na Huduma ya Uinjilisti ya Neema (Grace Evangelistic Ministries)] kwamba Mungu atufungulie mlango kwa lile neno lake, tuinene siri ya Kristo, ambayo kwa ajili yake nimefungwa (Wakolosai 4:3).

Sera Za Kifedha

"... Mmepata bure, toeni bure." (Mathayo 10:8b)

Mungu anatoa mafundisho ya Biblia katika Neema ya ukuu wake, nasisi tunatamani kufuata nyayo za Neema. Kwa hivyo, hatulipishi gharama ya uchapishaji kutoka kwa hudumu hii. Mtu yeyote ambaye angependa kupokea vitabu, kanda na nakala nyingine, atavipokea bila malipo au sharti lolote lile.

Huduma ya Uinjilisti ya Neema (Grace Evangelistic Ministries, Inc.) inaendesha shughuli zake kwa matoleo ya hiari. Hatulipishi kwa ajili ya uchapishaji na hatuna orodha ya malipo kwa ajili ya uchapishaji. Hatuombi fedha. Ikiwa shukrani kwa ajili ya neno la Mungu itamtia motisha mwaminio kutoa, anao uhuru wa kuchangia kwa kueneza mafundisho ya Biblia.

Tuandikie

Ikiwa ungependa kupokea kijitabu hiki, na vitabu vingine vya kimsingi ambavyo vitakusaidia katika maisha yako ya kiroho, pasipo na malipo yoyote ile, tuandikie kwa moja wapo ya anwani zifuatazo:-

1. **Grace Covenant Church,**
   P.O. Box 4050-0020,
   NAIROBI, Kenya
   +254 722 737 495,
   +254 733 633 035

2. **Grace Evangelistic Ministries,**
   P.O. Box 992,
   BUJUMBURA, Burundi

3. **Grace Evangelistic Ministries,**
   P.O. Box 583,
   JOS, Plateau St. Nigeria

© 2004 Moses C. Onwubiko.
Haki zote zimeifadhiwa.
www.GEMworldwide.org

© 2009 Grace Covenant Church.
Nakala hii ya Kiswahili imetafsiriwa na kuchapishwa Nairobi, nchini Kenya, na kikosi cha wachungaji wataalamu wa Kiswahili.
www.gcckenya.org